# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA SITA

**06 NOVEMBA, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 06 NOVEMBA, 2023

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa

Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**69. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inazingatia vigezo gani kugawa Fedha za Mfuko wa Jimbo.

**70. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Stendi ya kisasa katika Mji wa Mwanga.

**71. MHESHIMIWA KASALALI EMMANUEL MAGENI (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuanzisha Halmashauri ya Wilaya ya Sumve ili kusogeza huduma kwa Wananchi.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**72. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini Serikali imewaacha Wananchi wengi wenye sifa na vigezo vya kunufaika na TASAF katika Jimbo la Mwibara.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**73. MHESHIMIWA SIMAI HASSAN SADIKI (NUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, sababu zipi zimekwamisha ujenzi wa ukuta maeneo yanayoathiriwa na Bahari Nungwi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**74. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kwa nini ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Kijiji cha Mwagwila haukamiliki ingawa Serikali imepeleka fedha nyingi.

**75. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaongeza bei ya zao la Chai ya Rungwe kutoka Shilingi 340/= hadi 700/= kwa kilo kutokana na kupanda gharama za uzalishaji.

**76. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani kutumia eneo la uwekezaji Kisasiga - Bukene kutengeneza *Block Farms* kwa ajili ya kilimo cha Alizeti.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**77. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukipandisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa kuwa Chuo Kikuu Kamili.

**WIZARA YA AFYA:**

**78. MHESHIMIWA ZAINAB ATHUMAN KATIMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi itaanza kujengwa.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA
UHURU NA UMOJA

## WIZARA YA MAJI:

**79. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Wananchi wa Kata za Nalasi Tunduru watapata maji ya uhakika.

**80. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi mkubwa wa Bilioni 41 wa kupeleka maji safi Ngara.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**81. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni haja ya kurejesha kwa Wananchi eneo la Namajani - Masasi kwa vile Jeshi la Magereza limeshindwa kuwalipa fidia.

**82. MHESHIMIWA STANSLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini jengo la Mahabusu katika Gereza la Maswa litakarabatiwa.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**83. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itafanya mapitio ya viwango vya malipo ya ujira kwa Wapagazi, Wapishi na Waongoza Watalii Mlima Kilimanjaro.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**84. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa ardhi kati ya Mwekezaji wa Shamba la Malonje na Wananchi wa Kata ya Muungano na Mollo Kwela.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**85. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO (SENGEREMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itakarabati Viwanda vya kuchambua Pamba vya Nyakarilo, Nyamirilo na Buyagu vilivyopo Sengerema.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**86. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Msalala.

## IV. KAMATI YA MIPANGO:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **06 NOVEMBA, 2023** | **KATIBU WA BUNGE** |